

Kwa mawasiliano zaidi;



Afisa Mtendaji Mkuu, Wakala wa Vipimo
Jengo la NSSF (Mafao), Gorofa ya Saba – Mtaa wa
Uhuru, Ilala)

S.L.P 313, Dar es Salaam.
Simu : +255 (022) 2203199,
Nukushi : +255 (022) 2203200,
Barua pepe : info@wma.go.tz,
Tovuti : www.wma.go.tz



WAKALA WA VIPIMO



**TAMBUA KISHERIA
MAMBO YA
KUZINGATIA KATIKA
MATUMIZI YA MIZANI**

Wakala wa Vipimo ni mojawapo ya Wakala za Serikali ambayo ilianzishwa tarehe 13 Mei, 2002 kwa Tangazo la Serikali namba 194 la tarehe 17 Mei, 2002. Awali, ilikuwa ni Kitengo chini ya Idara ya Biashara Wizara ya Viwanda na Biashara. Lengo la Serikali kuanzisha Wakala wa Vipimo ilikuwa ni kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

DIRA YA WAKALA WA VIPIMO

Kufikia viwango vya kimataifa katika utoaji huduma kwa jamii kupitia matumizi sahihi ya

DHIMA YA WAKALA WA VIPIMO

Kuthibiti vipimo vyote vinavyotumika na vinavyokusudiwa kutumika katika sekta ya Biashara, Mazingira, Afya na Usalama na kuelimisha umma kuhusu masuala ya vipimo nchini



Mizani aina ya Counter inayotumika kupimia bidhaa mbalimbali

MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA MATUMIZI YA MIZANI KWA MFANYABIASHARA

- Mfanyabiashara kabla ya kununua mizani ni lazima akague kama umehakikiwa na Wakala wa Vipimo na una chapa ya serikali au kubandikwa sticker ya mwaka husika,
- Mizani hupigwa chapa mara baada ya kukaguliwa na kuonekana upo sahihi, na ukaguzi huo ni mara moja kila baada ya miezi kumi na mbili (12).
- Mfanyabiashara anawajibika kuipeleka mizani isiyo na chapa katika ofisi ya vipimo iliyokaribu naye kwa ajili ya kuhakiki usahihi wake na kupigwa chapa.



Maafisa Vipimo wakiwa katika zoezi la mwaka (annual re-verification) wakihakiki vipimo vinavyotumika kuhakiki vipimo vya wafanyabiashara

Kama mizani itakuwa na hitilafu

- Mtumiaji yamlazimu aipeleke kwa fundi mizani kwa ajili ya marekebisha,
- Baada ya kurekebisha, fundi itamlazimu kuipeleka mizani Ofisi ya Vipimo kwa ajili ya uhakiki,
- Baada ya Wakala wa Vipimo kuthibitisha usahihi wa mizani hiyo na kuipiga chapa, mtumiaji ataruhusiwa kuendelea kuitumia katika biashara



Waombaji wa leseni za ufundi mizani wakifanya mtihani ili kupimwa uelewa wao

MAMBO YASIYORUHUSIWA KISHERIA KWA MATUMIZI YA MIZANI WA BIASHARA

- Muuzaji asipime bidhaa kwa kificho, hivyo inampasa apime bidhaa hiyo mteja akiwa anaona,
- Muuzaji asiweke jiwe kwenye mizani wakati mizani hiyo haitumiki mpaka pale atakapoanza kumpimia mteja,

- Muuzaji asiwashe feni kwa kasi wakati wa kumpimia mteja bidhaa,
- Hairuhusiwi mizani na mawe ya mfanyabiashara kuwa katika hali ya uchafu,
- Muuzaji haruhusiwi kumpimia mteja mzani ambao haujabalansi,



Meneja wa Mkoa wa Lindi Bw. Steven Masawe akitoa elimu kwa wananchi ambao walitembelea banda la Wakala wa Vipimo katika maonesho ya Wakulima (Nanenane) yaliyofanyika Mkoa wa Lindi mwaka 2014

ZIFAHAMU HAKI ZA MNUNUZI KATIKA MATUMIZI YA MIZANI

- Mnunuzi ana haki ya kuikagua mizani na mawe kwa kuangalia mhuri kabla hajapimiwa bidhaa
- Mnunuzi ahakikishe mizani haelemei upande mmoja
- Mnunuzi akihisi kama kuna udanganyifu wowote atoe taarifa kwa Wakala wa Vipimo kwenye ofisi ya Mkoa iliyokaribu naye (Wakala wa Vipimo ina Ofisi katika Mikoa yote Tanzania Bara isipokuwa mikoa mipya)

